

Matatizo ya Tafsiri katika Kazi za Fasihi: Tajriba Yangu Kutokana na Tafsiri ya *Othello-Tanzia* ya Mtu Mweusi

Ayub Mukhwana
Chuo Kikuu cha Nairobi

Ikisiri

Tamthilia ya *Othello* ni moja katika tamthilia pendwa za mwandishi maarufu wa Kimagharibi William Shakespeare. *Othello* ni moja katika tamthilia chache za Shakespeare zilizotafsiriwa kwa Kiswahili. Tamthilia zingine za Shakespeare zilizotafsiriwa kwa Kiswahili ni Juliasi Kaizari na Mabepari wa Venisi zote na Mwalimu Julius Nyerere. Makala haya yanahoji kwamba uchache wa tafsiri za vitabu vya Shakespeare unatokana na matatizo ya tafsiri yanayomkumba mtafsiri katika shughuli ya tafsiri. Lengo la makala haya ni kubaini matatizo ya tafsiri yanayomkumba mtafsiri wa kazi za fasihi kwa kurejelea tafsiri ya Kiswahili ya tamthilia ya *Othello*.

Maneno Muhimu: *Tafsiri, Fasihi tafsiri, Matatizo ya tafsiri, Othello.*

Utangulizi

Tafsiri ya *Othello: Tanzania ya Mtu Mweusi* ilichochea na mambo kadhaa. Kwanza ni kuhusu mwandishi wake asilia. William Shakespeare ni mwandishi maarufu sana katika taaluma ya Fasihi ulimwenguni kote. Kutokana na umaarufu wake, kazi zake nyingi zimetafsiriwa katika lugha nyingi kuu ulimwenguni, ikiwemo Kiswahili. Hata hivyo, tamthilia ya *Othello* inayomzungumzia hasa mtu mweusi haikuwa imetafsiriwa kwa Kiswahili. Hali hii kwetu tumeiona kama iliyo ya kinaya na ni sababu nyingine mojawapo iliyotia motisha tafsiri hii. Suala kuu la mapenzi limezungumziwa katika tamthilia yenyewe. Hii ni mada ambayo imekishughulisha kizazi cha mwanadamu kwa karne zote na itazidi kuwa muhimu; yafaa kuangaliwa katika ulimwengu wa Kiswahili kupitia tafsiri hii hasa sasa ambapo UKIMWI unauhangaisha ulimwengu.

Vile vile, lugha ni kitu kipanuzi ambacho hubadilika kila uchao. Hivyo basi, matini katika lugha za awali huenda yakose kuelewaka na watu wanaofahamu lugha za sasa. Hivi ndivyo pia kilivyo Kiingereza cha Shakespeare. Njia mojawapo ya kuyafanya yaliyomo katika Kiingereza hiki cha Shakespeare kueleweka ni kupitia kwa tafsiri. Hili ndilo lililokuwa lengo la tafsiri ya *Othello: Tanzania ya Mtu Mweusi* kutoka Kiingereza hadi Kiswahili. Ni muhimu kutaja kwamba makala haya ni ya kinadharia zaidi kuliko ilivyo kimatendo.

Kabla ya kuyachunguza, kuyaeleza na kuyajadili kwa kina matatizo ya tafsiri kama tulivyoyashuhudia katika kutafsiri tamthilia ya *Othello: Tanzania ya Mtu Mweusi*, hebu tueleze historia fupi ya Msanii huyu. Kwa kuelewa historia ya William Shakespeare, tutaweza kuelewa, japo kidogo, sababu zake za kuandikia maudhui aliyoyashughulikia, muundo wa lugha alioutumia na hata mtindo wake wa uandishi. Mambo haya ni muhimu katika kazi ya kisanii hasa inapohusishwa na tafsiri.

William Shakespeare

William Shakespear ni mwandishi anayetajika sana ulimwenguni kote. Anafahamika sana kama mwandishi mashuhuri aliyandika kazi lukuki za sanaa, hasa tamthiliya, wakati wake. Nyingi ya kazi zake zimetafsiriwa katika lugha nyingi za ulimwengu. Kwa mfano, tamthilia hii ya *Othello* imetafsiriwa katika lugha ya Kichina (Oseluo). Kazi alizoziandika zilizusu mawanda yote ya maisha katika mazingira aliyoyaishi. Ni kazi zinazoonyesha ubunifu wa hali ya juu ambao unamdhihirisha sio tu kama mwandishi mwenye kipawa, lakini pia kama mwandishi mwenye bidii na ambaye alitia azima kuelewa jamii yake na pia kuielimisha huko akishesha na kukashifu. Tamthiliya ya *Othello* imechukua mkondo huu.

Kuna stakabadhi za kuaminika ambazo zinaeleza kwa kina juu ya maisha yake kuanzia mwaka wa 1592. Inakisiwa kwamba Shakespear aliandika zaidi ya tamthiliya arobanne. Kati ya kazi zake hizi, inaaminika kuwa kazi yake ya kwanza ilikuwa *Venus and Adonis* (1593). Hatimaye aliandika tamthiliya nyingi zinazotajika hadi leo zikiwemo *Romeo and Juliet*, *The Merchant of Venice*, *Julius Caesar*, *Hamlet*, *Othello*, *Macbeth* kati ya zingine. Baadhi ya tamthiliya hizi zimetafsiriwa hadi Kiswahili nazo ni *Juliasi Kaizari*, *Mabepari wa Venisi* na *Othello: Tanzania ya Mtu Mweusi*.

Kufikia mwaka wa 1596, Shakespear alikuwa amepata utajiri wa kutajika na akaweza kununua jumba la kifahari lililoitwa “New Place” kwa Pauni 60, pesa nyingi sana wakati huo. Pia, kupitia kwa babake, aliweza kununua nembo ya taifa na hivyo yeye na aila yake wakawa wametambuliwa rasmi kama “waungwana”. Kufikia mnamo 1598, Shakespear ndiye aliyetambulika kama mwandishi na mwigizaji hodari na bora kabisa wa tamthiliya na kazi zake zikawa zinachapishwa kwa wingi.

Kuanzia mwaka wa 1601, Shakespear hakuandika sana kama alivyofanya awali na inaelekea kuwa kufikia mwaka wa 1607, Shakespear aliacha kuigiza kwa kuwa jina lake halikuonekana katika orodha za waigizaji baada ya 1607. Kuanzia wakati huo, Shakespear aliishi jijini Stratford kama mstaafu. Huko, alipewa hadhi kuu kama mtu mashuhuri. Hata hivyo, alikuwa akiandika tamthiliya japo si kwa wingi. Katika miaka minne ya mwisho ya uhai wake, Shakespear alikuwa amestaafu kutoka kwa uandishi kabisa.

Dhana ya Tafsiri

Tafsiri ni elimu inayohusu utoaji wa maelezo ya lugha fulani hadi lugha nyingine kimaandishi. Yaani, dhana ya tafsiri huandamana na mawasiliano kimaandishi kutoka lugha moja asilia au chanzi hadi lugha nyingine pokezi. Hii ni tofauti na ukalimani ambapo kunakuwa na tafsiri ya papo kwa papo kimazungumzo.

Tafsiri ni taaluma yenye uhusiano mkubwa na taaluma zingine nyingi. Kwa hali hii, tafsiri inaweza kufasiriwa kwa namna mbalimbali kutegemea miegemeo ya kitaaluma. Hata hivyo, kwa jumla tafsiri ni mahusiano yaliyopo baina ya makala asilia na makala zalishwa. Mahusiano haya yaweza kuwa ya karibu au ya mbali lakini kwa vyovyote vile, tafsiri yaweza kuwa ama imefaulu au imepotoshwa kutegemea masuala mengi ya kijamii, kitamaduni, kisiasa, kihistoria, kisera, na kimbeko. Ni kwa misingi hii wasomi wa tafsiri wataziegemea dhana za *ulinganifu* na *uafaafu* wanapozihakiki kazi zilizotafsiriwa. Hizi dhana zinaturegesha pale pale pahasupo namna kazi iliyotafsiriwa inahusiana na kazi asilia. Japo hivi ndivyo inavyoelekea kuwa, twafaa tujiulize ni kwa kiasi gani kazi hizi mbili zahitaji kuhusiana na kuzalisha taathira zitakazodhihirisha kama zinazoshughulikia tamaduni mbili tofauti tukizingatia kuwa ni lugha mbili na hata nyakati mbili tofauti zinazohusika.

Fikira hizi kuhusiana na tafsiri kama taaluma zimetupitikia wakati tukifanya tafsiri ya kitabu hiki. Baadhi ya maswali tuliyojiuliza ni: *Je, tafsiri hulengwa wasioelewa lugha asilia? Je, makala iliyotafsiriwa huruhusiwa kutaja mambo ambayo hayamo katika makala asilia? Je, visawe vina maana sawa katika kazi za tafsiri? Na Je, wakati wa kutunga kazi asilia na ule wa kutafsiriwa vitaletaje mtafaruku katika thamani ya tafsiri?* Katika kujibu maswali haya magumu, tulitilia maanani suala la mielekeo na itikadi zetu mbali na kuzingatia tofauti katika miundo ya lugha tulizoshughulikia na utanzu wa fasihi unaohusika na jinsi mtunzi wa kazi asilia alivyotunga. Jambo muhimu na la msingi ni kukumbuka kuwa, juu ya mengine yote, huu ni mchezo wa kuigizwa.

Kama mtafsiri aliye na misingi, japo hafifu, katika fasihi, nilifahamu tosha tangu mwanzo kuwa msomaji wa kazi za ubunifu au bunilizi kama hii huwa na matarajio mengi sana kutoka kwa mtafsiri. Msomaji wa kazi za kisanii kama hii atatarajia tafsiri ambayo ni nzito kama ilivyo kazi asilia au hata zaidi na ambayo yafaa kubadili kitu fulani kwa namna msomaji atakavyojiona na kujihisi kama mwanajamii. Mbali na hili, msomaji wa kazi za kisanii ambazo zimetafsiriwa anatarajia kuburudishwa na hata kupumbazwa na kazi zilizotafsiriwa na burudani hili latarajiwa kuwa ni la kiakademia. Ili mtafsiri wa kazi za kisanii aweze kutosheleza haya masharti mazito na yaendayo na matarajio ya wasomaji, mtafsiri sharti awe na uelewa wa hili jambo la kimsingi, aimudu lugha tafsiriwa barabara, huku akizingatia mirindimo na urari wa kisanii unaohitajika na vile vile kuifahamu misemo, semi, ndumo na mizungu mingine yote ya lugha inayoendana na lugha zote mbili.

Mjadala kuhusu Tafsiri kama Taaluma

Mmoja katika watu ambao wamefanya kazi hii ya tafsiri ni mwanaisimu Nida. Yeye alishughulikia lugha za Marekani akiangalia matatizo yanayomkumba mtafsiri. Hili alilifanya kijumla kwa kuangalia mambo mbalimbali yawezayo kuileta hali hii ya matatizo kwa mtafsiri. Hivyo, Nida alisema kuwa kutafsiri kuna matatizo mbalimbali. Aligundua kwamba:

1. Ni vigumu kuzungumza juu ya lugha bila kuinasibisha na utamaduni wake (Nida 1964). Hii ni kwa sababu kuwa lugha ndicho chombo cha kuelezea utamaduni wa watu fulani. Kifaa fulani cha utamaduni kinapokuwa miongoni mwa watu fulani, neno la kukitajia kifaa hicho litakuwa katika lugha hiyo husika. Yapo machukulio kuwa lugha za mnasaba mmoja zina ukaribu wa kitamaduni na kwa hiyo inakuwa rahisi kutafsiri matini yake kuliko zile ambazo hazina mahusiano ya kinasaba. Japo huu ni ukweli, kwa kiasi fulani ukweli huu unaweza kupotosha tafsiri. Hii ni kwa sababu etimolojia za maneno pekee haitoshi. Yapo maneno ambayo yanakuwa na uhawilishi wa maana na kwa hiyo yanaweza kupotosha tafsiri. Pia ifahamike kuwa kamusi pekee haiwezi kamwe kufaulisha tafsiri na kuifanya iwe bora. Hili pia laendana na miongozo mingi iliyoandikwa kuhusu tafsiri nzuri. Miongozo hii ni kama Biblia au Kur’ani ambazo kamwe haziwezi kumfanya mtu kuwa Mkristo au Mwislamu mzuri mtawalia.
2. Hakuna utamaduni hata mmoja ulimwenguni ambao haukuathiriwa na utamaduni mwingine. Hii ni kwa sababu utamaduni ni kitu kipanuzi ambacho hubadilika kila uchao kutokana na maingiliano baina ya watu wenye kutumia lugha tofauti tofauti katika mawasiliano yao. Watu fulani wanapokuwa na kifaa fulani cha kitamaduni huku wengine hawana, njia mojawapo ya kuonyesha mahusiano yao ni kwa utamaduni mmoja kukopa neno la kutajia kifaa husika kutoka kwa mwingine. Kimsingi, lugha ambazo zimekuwa na mahusiano ya muda zinarahisisha shughuli ya tafsiri kinyume na zile ambazo hazijawa na maingiliano au mahusiano yoyote.

Mawazo kama haya yalikuwa yamefikiriwa na wataalamu kama vile Whorf (1950). Whorf alisema kuwa kila utamaduni unajitosheleza na kujisimamia na pia huathiriwa na mazingira. Usemi huu wa Whorf una maana kuwa si haki kuusema utamaduni fulani kuwa ni duni au bora kuliko mwingine. Mawazo Whorf yalichochea na mawazo yaliyosambaa sana Ulaya na yaliyodai kuwa utamaduni mzuri ni ule uliopatikana Ulaya. Sura, akili na lugha za watu wengine kutoka sehemu zingine ulimwenguni zilipuuzwa ikilinganishwa na zile za Ulaya. Hii inamaanisha kuwa utamaduni wao pia ulipuuzwa.

Fikiria hizi zilijengeka katika mawazo ya Darwin (1859) na falsafa yake kuhusu *Chanzo cha Kizazi*. Kwake Darwin, binadamu aliibuka kuwa namna alivyo kupitia kukua hatua. Kwa hiyo, baadhi ya wachunguzi waliuchukua huu “udawini”,

wakautanua na hata kuzungumza juu ya “udawini” wa Kijamii. Kwa mujibu wa huu “udawini”, hata jamii, utamaduni, na ustaarabu wa watu hukua hivi hivi. Huu “udawini” wa Kijamii uliweka utamaduni wa Ulaya juu ya tamaduni zingine zote; nao ule wa Mwafrika ukawekwa chini kabisa. Mawazo haya pia yaliziathiri fikira za watu hawa kuhusiana na suala la lugha. Hii ni kwa sababu kwamba haiwezekani kamwe kuwepo utamaduni pasi na kuwa na lugha ya kuelezea; na pia lugha ni sehemu ya utamaduni. Basi, zile lugha za watu wa hali ya chini pia zilichukuliwa kuwa ni za hali ya chini.

Whorf akitoa mfano wa Kinavajo kutoka Marekani alisema kuwa bila kuathiriwa na taasubi zozote, baadhi ya lugha zinazodharauliwa zinao uwezo wa kueleza baadhi ya mambo vizuri zaidi kuliko zile za Ulaya. Pia, alisema kuwa kila utamaduni hujitoshesha na haipaswi kusema juu ya utamaduni fulani kwa kutumia kigezo cha lugha nyingine au utamaduni mwingine.

Mawazo yaliyokaribiana na haya yalibebwa na Malinowski aliyesema kuwa haiwezekani kueleza utamaduni wote ule bila kuwa na mtu aliyetoka katika jamii inayohusika au kujifunza lugha zenye kubeba tamaduni hizo. Mawazo haya ya Kianthropolojia yalikuwa na nguvu sana kiasi cha kupata wafuasi wengi.

Ingawa mawazo haya ya akina Whorf na Malinowski yalikuwa na mashiko, yanayo matatizo hapa na pale. Kwa mfano, hakuna kitu chochote kiunganishacho tamaduni mbili kwa mujibu wa yale anayoyasema Whorf. Kinachojitokeza katika fikira kama hizi ni kuwa tamaduni haziathiriani. Hata hivyo, ijulikanavyo ni kuwa tamaduni hukopa vifaa, na mawazo. Hii ndiyo maana Nida akasema kuwa matatizo ya tafsiri hutokana na tamaduni kutofautiana na pia kuwepo kwa athari mbalimbali zinazokwenda na tamaduni hizi. Mbali na tofauti za tamaduni kusababisha matatizo katika tafsiri kama shughuli, pia kuna suala la tofauti za mazingira na tofauti za miundo ya lugha zinazohusika katika tafsiri.

Tofauti hizi ziletazo ugumu katika tafsiri zaweza kuelezwa hivi:

Ulimwengu umegawika katika sehemu nyingi. Zipo sehemu zilizo za baridi, za joto, tambarare, na miti mikubwa. Hii ina maana kuwa ni mazingira yafanyayo watu kuwa na tofauti za majina na maneno katika lugha mbalimbali. Baadhi ya lugha zina ukwasi wa maneno yanayoeleza miti hali zingine hazina msamiati mwingi wa miti. Zile lugha zilizo katika mazingira ya wanyama zina ukwasi wa maneno ya wanyama. Mfano mzuri unaotolewa ni wa lugha ya Eskimo iliyo na maneno karibu manane yanayoeleza aina mbalimbali za barafu. Hali hii inatokana na ule utamaduni wa Waeskimo ambao unatokana na baridi. Wamaasai wa Afrika Mashariki nao wanao msamiati mwingi unaofungamana na ufugaji na hili pia linatokana na utamaduni wao unaoegemezwa kwenye mifugo. Jamii za pwani huwa na msamiati mpana unaohusu uvuvi na viumbe wa majini kinyume na jamii za sehemu jangwa.

Kila jamii hujiunda kwa namna yake ya kipekee. Kunazo jamii ziongozwazo na wafalme; na zipo jamii ziongozwazo na mabaraza ya wazee. Hali hizi pia huenda

sambamba na hali ya miundo ya kijamii. Kila muundo wa kijamii unao muundo wake wa kisiasa, uongozi, na imani zake ambayo ni mambo yanayotofautiana na ya jamii zingine. Mambo haya yote huchangia katika kusababisha matatizo ya tafsiri. Hii ni kwa sababu mambo haya huleta matatizo katika kupata maneno mwafaka kutoka lugha asilia ya makala ya tafsiri hadi pokezi. Kisha kunalo suala la tamaduni kubadilika kila uchao. Suala hili husababisha mabadiliko katika lugha na kufanya maneno mapya kuundwa ili kukidhi mahitaji ya hali hii ya mambo yanayobadilika. Kwa kuwa lugha na utamaduni ni vitu ambavyo huendelea kubadilika, tunaweza kuzungumza juu ya utamaduni wa watu fulani kwa kipindi fulani tu cha wakati. Hivyo basi mapisi ya wakati ni kikwazo kingine kiletacho utata katika shughuli nzima ya tafsiri.

Tatizo jingine la tafsiri hutokana na tofauti za miundo ya lugha (Nida 1964, Beekman na Callow 1974, Cartford 1965). Yaani, lugha zote za ulimwengu huweza kuwekwa katika makundi tofauti kwa matumizi ya vigezo mbalimbali. Kwa mfano, kuna lugha za Kiafrika, za Bara Hindi, za Ulaya, na za Marekani ya Kusini. Huu uainishaji lugha umefanywa kwa misingi ya maeneo ya kijiografia na pia kwa mujibu wa uhusiano wa kimuundo. Lugha zikiwa zimehusiana kimuundo, kwingi zinakuwa ni za asili moja ambapo asili ile inazipa kuwa na msamiati unaokaribiana au kuelekeana. Lugha zikiwa hivi, huwa ni rahisi zaidi kutafsiri baina ya lugha hizo kuliko zile ambazo hazikaribiani. Tatizo hili kuhusu muundo wa lugha katika tafsiri hujitokeza pia pale ambapo tafsiri inafanywa kutoka lugha moja yenye mofimu za lakabu (jenda) za kike au kiume hadi ile ambayo haina. Kwa mfano, sentensi ya Kiingereza *He came* inapotafsiriwa kama *Alikuja* katika Kiswahili inadhihirika wazi kuwa tafsiri hii haikupiga ndipo. Anayeitafsiri tena sentensi hii ya Kiswahili hadi Kiingereza atashindwa kujua kama aseme *She came* au *He came*. Katika hali hii, jenda haibainiki.

Kwa kuzingatia muundo wa lugha pia, kunazo lugha ambazo zina mpangilio huru wa maneno katika vifungu au sentensi hali zingine hazina mpangilio kama huo. Mfano wa lugha kama hizi ni Kirusi. Hali hii pia huenda na lugha zijulikanazo kama lugha-tenganishi ambazo hudhihirisha maana za kile kinachosemwa kutokana na mpangilio wa maneno katika tungo au sentensi. Kisha kunazo lugha zinazozingatia shadda au mkazo ambao waweza kuwa huru au funge. Lugha ya Kiingereza ni mfano wa lugha yenye mkazo huru. Kutokana na hali hii, mtu anaweza kujikuta kakanganyika anapoulizwa kutafsiri neno *Advise* kutoka Kiingereza hadi Kiswahili. Kimsingi, tofauti hizi katika muundo wa lugha ulimwenguni huweza kusababisha matatizo katika kutafsiri kutoka lugha moja hadi nyingine.

Matatizo ya tafsiri yaliyo ya kilugha hutokana na ile hali ya lugha kukopa msamiati kutoka lugha zingine. Kuhusu suala hili la ukopaji wa msamiati, kuna wakati ambapo lugha fulani yaweza kuwa changizi au lugha pokezi. Lugha husika hupata umuhimu fulani kwa sababu za siasa, sheria, na uchumi. Vivyo hivyo tamaduni jirani zitakopana sehemu fulani za kitamaduni. Pia, kutumika kwa lugha

ya Kiyunani na Kiarabu kwa muda mrefu kumezifanya ziathiri jamii nyingi sana ulimwenguni. Nayo lugha ya Kiingereza imeziathiri lugha nyingi kimsamiati kwa sababu ya kusambaza ukoloni wao pamoja na teknolojia.

Hapa tatizo la tafsiri linajitokeza kwa sababu katika akili za baadhi ya watafsiri na watafsiriwa, haijulikani wazi ikwa maneno yaliyokopwa yaitwe ya kigeni au ni maneno ya lugha lengwa katika tafsiri. Yafaa ieleweke kuwa hapana lugha ulimwenguni ambayo haijakopa msamiati kutokana na mahusiano na maingiliano baina ya wenye kutumia lugha mbalimbali katika mawasiliano. Hata hivyo, athari za lugha fulani kwa nyingine huwa hivi katika muktadha fulani tu na wala si katika miktadha au nyanja zote za maisha.

Katika sehemu hii, tumesema mengi kuhusu tafsiri na kwa maoni yetu, hali hii ndiyo ifaayo kufikiriwa kama nadharia ya tafsiri. Hii ni kwa sababu nadharia yoyote nzuri huanza kwenye kutambua na kueleza matatizo yanayokumba taaluma fulani au kitengo chake, na katika muktadha huu tafsiri. Hii ni kumaanisha kuwa nadharia ya tafsiri hujumuisha masiala yote yafaayo kuzingatiwa katika kutatua matatizo ya tafsiri. Nadharia hii ya tafsiri huweza kuorodhesha uwezekano wote wa jinsi ya kutafsiri. Hatimaye, nadharia ya tafsiri yafaa ipendekeze jinsi ya kutafsiri iliyo nzuri zaidi ya zote ili kuzalisha tafsiri nzuri ya zote. Kwa hivyo, hakuna nadharia ya tafsiri bila ya nadharia hiyo husika kutumikizwa. Kama ilivyo katika taaluma zingine, mbali labda na dini, hapana sheria funge katika tafsiri na ndio maana hamna nadharia moja pekee na iliyo kamilifu ya tafsiri.

Ili kuweza kutafsiri, yafaa mtafsiri awe na uwezo wa kusoma na kufahamu lugha zinazohusika. Hii ni kwa sababu kile kilicho muhimu katika tafsiri ni matokeo. Hivyo basi inambidi mtafsiri awe ni mwenye kuchangamkia na pia kuelewa mada ambayo anatafsiri. Kutokuwa na uelewa wa mada inayotafsiriwa kutapelekea kujitokeza kwatafsiri iliyo na makosa madogo madogo ambayo yangeepukwa.

Mbali na ukweli huu, yafuatayo ni baadhi ya masiala muhimu yafaayo kuzingatiwa wakati wa kutafsiri:

1. Mwandishi wa lugha asilia yuafaa kutiwa maanani (Brower 1966). Hii ina maana kuwa, kwa kuwa kila mwandishi anao mtindo unaomsawiri yeye kama yeye, mtindo wa mwandishi wa kazi asilia hauna budi kutiwa maanani. Kwa kuwa kila mwandishi ana namna yake katika maandishi yake, namna hii yafaa ihifadhiwe katika tafsiri. Kwa kuzingatia hili, kazi iliyotafsiriwa itajitokeza kama iliyo ya kuchochea hisia kama ile asilia kiasi cha kuweza kusomwa au kuigizwa kama kazi ya sanaa na asilia. Hii ni kwa sababu kazi zinapotafsiriwa, kazi, jukumu na wajibu wa mtafsiri huwa ni kuunda upya kazi hii kwa namna inayogusa hisia za wasomaji, waigizaji au hadhira mpya iliyolengwa kazi ya tafsiri.

2. Kaida za lugha asilia zafaa kuzingatiwa katika tafsiri. Kaida za lugha asilia zilizo za kisarufi na kileksia zafaa zihifadhiwe katika tafsiri ifanywayo. Kwa mfano, zipo lugha ambazo muundo wa sentensi zake unaopendelewa kisarufi si wazi. Hali hii huwa hata na utata zaidi pale ambapo kazi ya kisanii inahusika na kwa hiyo mtunzi inayo idhini ya kishairi au uhuru wa kisanii. Mambo yawapo hivi mtafsiri hawezi kuanza tafsiri yake moja kwa moja bila kwanza kuelewa matini nzima na vile vile kutiwa kila kifungu katika muktadha wake mbali na kuzingatia mapigo ya kisanii yanayojitokeza katika vifungu mbalimbali na athari yake ya kijumla kwa kazi husika.
3. Utamaduni wa lugha asilia pia ni muhimu kutiwa maanani. Kwa mfano, kule Uingereza mbwa ni rafiki mkubwa wa binadamu. Hali hii ni tofauti na hali halisi ilivyo barani Afrika. Katika utamaduni wa Wamaori, nguruwe ni ishara ya utajiri, Ulaya nguruwe ni nyama lakini katika utamaduni wa Kiislamu nguruwe ni najisi na haramu. Kwa misingi hii, yule anayetafsiri sharti awe na utambuzi wa kuzitofautisha hali hizi za kitamaduni ili anapokuwa anatafsiri apate visawe katika lugha pokezi ambavyo havitapotosha maana au kuisimua na kuamsha hisia ziwazazo kuhasiri upokelewaji wa tafsiri husika.
4. Mandhari na desturi za kazi asilia ni sharti kuzingatiwa. Hii ni kumaanisha kuwa yafaa mtafsiri ajue jinsi kazi asilia ilivyotolewa kwa mara ya kwanza. Yaani, tafsiri kama shughuli huhusu ufanyaji maamuzi yasiyo kikomo huku suala la ukadiriaji wa yafaayo kizingatiwa na kutozingatiwa ukifanywa nia ikiwa ni kujitokeza na aina ya urari na mapigo ambayo kwingineko yangehasiri hata suala la sarufi na nia ya makala asilia. Haya yote yanafanywa ili kuipa tafsiri upekee wake huku viwango mbalimbali vya kazi asilia vyenye nia ya kuhifadhi matarajio ya mwandishi asilia vikizingatiwa. Yaani, tafsiri, hasa inayohusu kazi ya fasihi huhitaji kujitokeza na misepetuko pamoja na mirindimo na vile vile imani ya mwandishi asilia. Kwa hali hii, mtafsiri hana budi kutumia uwezo na muda wake vyema ili kujenga upya kazi asilia katika tafsiri yake.
5. Mbali na ukweli huu, kaida na mbeko za lugha lengwa sharti kuzingatiwa. Hii hali ni kwa lengo la kuhifadhi na kudumisha miiko inayopelekana na utamaduni wa hadhira lengwa. Kwa mfano, katika jamii nyingi za Kimagharibi ni jambo la utovu wa heshima na usimbeko kwa mama kuonyesha titi lake hadharani. Hali hii ni kinyume kabisa na ilivyo katika jamii nyingi za Kiafrika ambazo huweza kunyonyesha watoto hadharani. Hali kama hii vile vile inaweza kuleta utata katika upokelewaji wa jumbe kutoka lugha asilia hadi lugha pokezi katika shughuli ya tafsiri.
6. Utamaduni wa lugha lengwa wafaa kuzingatiwa katika uhawilishaji wa matini kutoka lugha asilia kuingia katika lugha hiyo pokezi. Jamii lugha mbalimbali hudhihirisha tamaduni tofauti tofauti. Ulimwenguni sasa, zipo jamii ambazo

zinapinga vikali sana suala la upashaji tohara kwa kina dada huku zingine zikichangamkia hali hii. Ni kwa misingi hii ambapo dhana za ukeketaji na upashaji tohara ambazo zilikuwa visawe miaka michache iliyopita zimejionyesha kama zilizo kinzani. Hili ladhihirisha kuwa utamaduni ni kitu kipanuzi ambacho daima ki mbioni kubadilika. Kwa hili, zipo jamii lugha zinazokubali mabadiliko haraka kuliko zingine. Hili laweza kuhasiri tafsiri lau kama halikuzingatiwa chini ya kipengele cha utamaduni.

7. Mandhari ya lugha lengwa pamoja na desturi zake ni muhimu katika tafsiri. Kwa kuzingatia vipengele hivi, ujumbe unaotafsiriwa utaweza kuifikia hadhira yake kwa mguso na mvuto uliokusudiwa. Japo tunaishi katika kijiji kutokana na utandawazi, sharti tukubali kuwa hata sasa yapo maeneo yanayoathiriwa na utandawazi kwa namna tofauti na mengine. Hali iwapo hivi kunayo mandhari tofauti tofauti na yenye uzoefu uliotofautiana. Katika tafsiri, mandhari tofauti tofauti yakizingatiwa upokezi utakuwa na mguso ulio na athari tofauti na makala asilia.
8. Walengwa wa tafsiri husika wafaa kutiwa maanani. Kwa kufanya hivyo, maswali kama haya yafaa kuulizwa: Je, walengwa wa tafsiri husika wanafahamu nini kuhusu kile kinachotafsiriwa? Je, matarajio ya walengwa wa tafsiri husika ni yapi? Maswali haya ni muhimu hasa inapokuja katika aina ya tafsiri ifaayo kuzingatiwa katika tafsiri kama taaluma. Mtafsiri yuafaa kujiuliza ikiwa tafsiri ya neno kwa neno itafaa hadhira yake au ni tafsiri maana au aina zote mbili na kwa matokeo gani ya kimawasiliano.
9. Ukweli ni muhimu katika tafsiri. Ukweli huu kuhusu tafsiri unatokana na yaliyomo katika makala au kitabu asilia na kinachotafsiriwa. Ukweli hauendani na hisia au mielekeo na taasubi ya mtafsiri au hata matarajio ya hadhira inayolengwa. Hapa hivi ni vyema kutofautisha baina ya dhana za urongo, ubunifu na ukweli. Daima ikumbukwe kuwa ubunifu ni kando kabisa na urongo.
10. Ni muhimu kukumbuka kuwa tafsiri ni mali ya lugha pokezi na hivyo mambo yanayohusu lugha hiyo pokezi yanafaa kupewa umuhimu zaidi. Kwa mfano, kila lugha hujiundia misemo, msamiati, maneno miko na mambo mengine ya muundo wa lugha kutegemea mazingira na mpangilio wake wa kijamii. Uandishi wa tafsiri kwa hakika unahusu uundaji wa matini mpya na inayojitegemea katika lugha pokezi. Hoja hii ina maana kwamba kihali halisi hatutegemei kuwa kazi ya tafsiri na ile asilia zitakuwa kama rupia kwa ya pili. Hii ni kwa sababu mwandishi wa lugha asilia na yule wa lugha pokezi wanaweza kutofautiana kwingi tu inapokuja kwenye mahusiko ya kijamii. Kwa hali hii kufaulu na (au) kutokufaulu kwa kazi ya tafsiri huathiriwa na masiala mbalimbali.

Kutokana na masiala haya, swali linaloweza kuulizwa ni: *Je, kila kitu chaweza kutafsiriwa?* Kufungamana na swali hili, je, utasemaje kuhusu teknolojia ya kompyuta katika lugha ya Kimaasai? Kumbuka kuwa yawezekana dhana na istilahi za kompyuta zisiwepo katika lugha hiyo ya Kimaasai kwa sasa. Pale ambapo dhana za kompyuta hazipatikani katika lugha ya Kimaasai, dhana hizi zaweza kuelezwa kwa maneno mengi na mtafsiri. Hatimaye, tafsiri kama hii inajitokeza kuwa ni kutoa maelezo. Katika hali kama hii, tafsiri itakuwa ndefu kuliko makala asilia na athari yake kwa msomaji itakuwa tofauti na ile ya makala asilia. Vile vile kila lugha ulimwenguni hujitosheleza kama chombo cha mawasiliano katika mazingira yake. Kwa hiyo, haja ya kukitafutia Kimaasai msamiati fulani inapotokea, msamiati huo utapatikana. Hapa vile vile tutofautishe msamiati katika ujumla wake na istilahi. Msamiati ni jumla ya maneno yapatikanayo katika lugha huku istilahi ukiwa ni msamiati maalumu unaokwenda na nyanja fulani maalumu. Kwa hali hii, si haki kudai kuwa lugha fulani haijitoshelezi kimsamiati bila kwanza kushauriana na wadau kwenye nyanja husika na vile vile wataalamu wa ukuzaji msamiati katika lugha.

Tunaishi katika ulimwengu wa utandawazi na uliojaa uguraji wa sehemu mbalimbali za ulimwenguni. Kwa sababu hii, watu wamefahamu tamaduni za wenzao huku vile vile wakipata mawazo mapya kutoka kwao mbali na kuwa na mikabala na mitazamo mbalimbali kuhusu maisha. Kutokana na ukweli huu, mtafsiri anapotafsiri kazi ya kisanii hana budi kuzingatia tofauti za kitamaduni na za kimawazo zipitikiazo watu wa maeneo mbalimbali na vile vile kutambua kuwa kumezuka ulimwengu mpya unaohitaji makini kukabili na kazi zilizotafsiriwa. Kwa mantiki hii, mtafsiri anakuwa ni kiungo muhimu katika mfanyiko wa kisanii huku mhariri wa kazi ya tafsiri akiwa ni mwenda-kati naye mchapishaji na msomaji wakiwa ndio walengwa wa kazi ya kisanii. Kwa hiyo ni muhimu kuwa mtafsiri pamoja na mhariri wawe ni watu wanaofanya kazi hii ya tafsiri kwa ushirikiano kiasi cha kila mmoja wao kuridhika na kutiwa hamasa na kazi ya mwingine. Mambo yawapo hivi, ushirikiano wao husaidia kuifanya kazi ya kisanii iwe ifaayo kutokana na kujitokeza na tafsiri iliyo nzuri na hili litafanywa kwa kufuata kitaratibu hatua zote za tafsiri na uhariri. Jambo hili litafaulu kuleta tafsiri iliyo nzuri kwa kulinda na kuhifadhi ubora na msimamo wa kazi asilia na wakati huo huo kujitokeza na kazi ya kisanii iwezayo kuihamasisha hadhira lengwa katika tafsiri husika.

Kazi ya tafsiri iliyo nzuri ni ile iwezayo kulandana na kazi asilia kiasi kwamba mbali na kuweza kuvutia kisanii iweze pia kuvutia kimuktadha (Mutie, 1997). Hii ni kumaanisha kuwa kazi ya tafsiri haina budi kuwa na uzuri, ulimbwende, mpangilio na mwonjo unaopatikana katika kazi asilia. Vile vile, kazi iliyotafsiriwa sharti pia iweze kueleweka na hadhira yake mpya mbali na kuwa na umaana kwenye ngazi zote. Kimsingi basi, tafsiri sharti iwe na maadili kama yale yapatikanayo katika matini asilia na kuweza kuhamasisha hadhira hiyo mpya. Hata hivyo, kazi ya tafsiri sharti iweze kumulika na kuakisi tofauti za kijamii na za

kitamaduni za jamii lugha husika huku ikijaribu kupata usambamba uliopo baina ya kazi asilia na kazi ya tafsiri. Kwa kufanya yote haya, kazi ya tafsiri sharti ijitokeze na usawazisho mwema baina ya tafsiri ya neno kwa neno na tafsiri maana. Vile vile hadithi katika tafsiri pamoja na maghani yake sharti viendane na yaliyomo katika kazi asilia. Mwisho, kazi ya tafsiri lazima iweze kusomeka na walengwa wayo katika lugha mpya na kwa namna ile ile na kwa uelewaji ule ule kama ambao umo katika matini asilia. Kama inavyojitokeza katika maelezo haya, kazi ya mtafsiri ni ngumu kwa kuwa inayo matarajio mengi mno.

Japo ni ngumu na tata, tafsiri kama taaluma ni muhimu sana katika mawasiliano kwa sababu zifuatazo:

1. Ripoti, magazeti, vitabu, n.k huhitaji kutafsiriwa ili watu kutoka jamii lugha mbalimbali waweze kujisomea.
2. Tafsiri hutumiwa ili kuhawilisha utamaduni wa watu fulani hadi kwa wengine (Rabin 1958). Kwa mfano, utamaduni wa Kiyunani ulifika Uingereza kupitia kwa tafsiri. Pia, vitabu vingi vya dini, kwa mfano Biblia, vimetafsiriwa kwa lugha nyingi tofauti na hivyo kuwafikia watu wengi katika tamaduni na maeneo mengi tofauti.
3. Tafsiri ni mbinu mojawapo ya ujifunzaji wa lugha za kigeni. Hii ni kwa sababu mtu aweze kuwa mtafsiri mzuri kama hafahamu vyema lugha zote zinazohusika.

Kimsingi, tafsiri hutumika kama nyenzo ya mawasiliano. Leo hii mawasiliano ni muhimu sana katika biashara, usafiri, diplomasia, siasa, usomi n.k.

Hitimisho

Zipo aina nyingi za tafsiri. Hata hivyo, hakuna aina moja ya tafsiri inayoweza kutazamwa kuwa ndio bora kuliko zingine zote. Aina ya tafsiri na pale ifaapo zaidi hutegemea masiala kama vile muktadha, mada, lengo, na walengwa. Hii ni kumaanisha kuwa katika kutafsiri tamthilia ya *Othello: Tanzania ya Mtu Mweusi*, changamoto mojawapo tuliyokumbana nayo ilihusu ni nadharia ipi itumike wapi na kwa athari gani kwa hadhira lengwa na ambayo vile vile si maalumu.

Mengi ya yale yaliyotajwa hapa kuhusu tafsiri kama taaluma yalitumiwa katika tafsiri hii ya *Othello: Tanzania ya Mtu Mweusi*. Kimsingi, matatizo ya tafsiri katika tamthilia ya *Othello* yalitokana na ukweli kuwa Kiingereza cha Shakespeare kina wingi wa maana za maneno. Kiingereza hiki na Kiswahili ni lugha zilizo tofauti kimuundo na kimsamiati, na vile vile kuna ugumu wa kutafsiri nahau na misemo iliyopitwa na wakati kutoka lugha asilia ya Kiingereza cha Shakespeare hadi lugha pokezi ya Kiswahili. Hili vile vile lilijitokeza kama changamoto iliyotukumba katika kutafsiri tamthilia hii ya Shakespeare.

Kazi ya Fasihi inapotafsiriwa kutoka lugha asilia hadi lugha pokezi au lengwa, nia yake hasa huwa ni kufahamisha umma wa lugha pokezi kuhusu kuwepo kwa

kitu fulani cha kifasihi katika kazi asilia. Kazi hii ya tafsiri hupelekwa kwa mhariri wa chumba cha uchapishaji vitabu ili naye aweze kutathmini ubora wa tafsiri husika. Hili hutokana na ukweli kuwa wahariri siku zote ni wataalamu lakini vilevile wanaongozwa na sera ya matibaa ya kutaka kupata soko kwa tafsiri husika mbali na kuhakikisha kuwa ni tafsiri nzuri. Kwa hali hii, sharti kuwe na hali ya kusawazisha na kuwastanisha utaalumu wa mtafsiri na ule wa mhariri wa kazi iliyotafsiriwa. Hili likifanyika, kutapatikana tafsiri ambayo itauza na vile vile ambayo ni aminifu kwa maono ya mwandishi na ubora wa kisanii. Hali hii yaonyesha basi kuwa mfanyiko unaozalisha tafsiri iliyofaulu ni uwezao kuleta madhara mengi kwa kazi asili na hili linaweza kuhasiri upokelewaji wa tafsiri husika na umma lengwa. Hata hivyo, tafsiri hufaulu kwa mtafsiri na hata mhariri wa tafsiri kuzingatia hatua zinazohusika na zinazohakikisha kuwa yafaayo kufanywa kuhusu tafsiri yanatekelezwa hatua kwa hatua kutoka mwanzo hadi mwisho mwa shughuli ya tafsiri. Hali hii vile vile ilijitokeza kama changamoto kwa kuwa mhariri alifanya mabadiliko si haba kwenye tafsiri asilia. Kwa mfano jina Othelo limeendelezwa kama kwamba si la Kiswahili kimuundo. Hata hivyo, kwa yote nabeba lawama hasa pale ambapo tafsiri hii inayo mapungufu.

Marejeleo

- Beekman, J. and Callow, J. (1974). *Translating the Word of God*. Grand rapids. Michigan: Zondervan Publishing House..
- Brower, R. A. (Mhr) (1966). *On Translation*. New York: Oxford University Press.
- Cartford, J. C. (1965). *A Linguistic Theory of Translation*. London: Oxford University Press.
- Darwin, C. (1859). *On the Origin of Species by Means of Natural Selection or the Preservation of Favoured Races in the Struggle for Life*. London: John Murray.
- Malinowski, B. (1944). *A Scientific Theory of Culture and Other Essays*. Chapel Hill, North Carolina: The University of North Carolina Press.
- Mutie, E. K. (1997). *Sanaa katika Tafhiri: Matatizo na Athari Zake. Tasnifu ya Shahada ya Umahiri*. Haijchapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Nida, E. (1964). *Toward a Science of Translating*. Leiden, Netherlands: E. J. Brill.
- Rabin, C. (Mhr.) (1958). *Aspects of Translation*. London: University of London Communication Research Centre.
- Whorf, B. L. (1956). *Language, Thought, and Reality: Selected Writings of Benjamin Lee Whorf*. Cambridge: MA MIT Press.

